TANGAZO LA SERIKALI NA. 556 la Tarehe 26/07/2019.

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28(1)(d))*

MAGU WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY ("MAGU WSSA") TARIFF ADJUSTMENT 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Magu (“Magu WSSA”), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa imeanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Magu WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 30 Septemba 2019 au kabla, Magu WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hili.

(b) Magu WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hili.

(c) Magu WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hili.

(d) Magu WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri la Bei

na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa.

Sura 414
Tangazo la Serikali na.193 la 2010

(e) Magu WSSA itapunguza upotevu wa maji kutoka 45% hadi 35% kwa mwaka 2019/20, 35% hadi 30% kwa mwaka 2020/21 na kutoka 30% hadi 28% kwa mwaka 2021/22.

(f) Magu WSSA itaongeza wastani wa masaa ya huduma kutoka saa 6 hadi saa 18, saa 20 na saa 22 kwa mwaka 2019/20, 2020/21 na 2021/22 mtawalia.

(g) Magu WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Magu WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Magu WSSA katika siku zijazo.

(h) kuanzia tarehe 1 Septemba 2019, Magu WSSA itaanza kulipa tozo ya EWURA kwa mujibu wa kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA, na kifungu cha 6 cha Kanuni za EWURA kuhusu Taratibu za Kukusanya ada na tozo.

Amri Na. 11-014

4. Amri hii inafuta Amri Na. 11-014 katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Magu (Magu WSSA).

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 3)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei ya sasa | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 300 | 1,100 | 1,250 | 1,400 |
| Taasisi | 335 | 1,300 | 1,390 | 1,480 |
| Biashara | 390 | 1,500 | 1,620 | 1,720 |
| Viwanda | 500 | 1,900 | 2,000 | 2,210 |
| Magati | 1,000 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| WatejaWakubwa | 390 | 1,500 | 1,620 | 1,720 |
| Wastani | 380 | 1,400 | 1,580 | 1,680 |

Jedwali Namba 1(b): Bei ya Sasa na Iliyoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei ya sasa | Bei iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 4,500 | Bei ya Maji kwa wateja wasio na dira zimeondolewa | | |
| Taasisi | 11,500 | | | |
| Biashara | 11,500 | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la wateja | Ada ya sasa | Ada iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 20,000 | Asilimia 20 ya Gharama za Maungansho kama Ilivyoelezwa katika Kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013. | | |
| Taasisi | 20,000 | | | |
| Biashara | 20,000 | | | |
| Viwanda | 100,000 | | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la wateja | Ada ya sasa | Ada ziliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 11,000 | 11,000 | 11,000 | 11,000 |
| Taasisi | 11,000 | 11,000 | 11,000 | 11,000 |
| Biashara | 11,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 11,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

Jedwali Namba 1(e): Tozo ya Sasa na Iliyodhinishwa ya Kuondoa Majitaka kwa Kutumia Gari ya Magu WSSA (Shilingi/Gari)

| Kundi la Wateja | TozoyaSasa | TozoZilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | - | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| Taasisi | - | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| Biashara | - | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| Viwanda | - | 50,000 | 50,000 | 50,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(b))*

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

| Kazi Zitakazofanywa | Shilingi Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Ukarabati na Ununuzi wa Vifaa | | | | |
| Kununua dira za Maji 1200 | 15.08 | 22.51 | 26.27 | 30 Juni 2022 |
| Jumla (UkarabatinaUnunuziwavifaa) | 15.08 | 22.51 | 26.27 | |
| UwekezajiMpya | | | | |
| Utanuzi wa Mtandao wa maji had iKinango, Mwamabanza na Kitongo | | 171.43 | 333.87 | 30 Juni 2022 |
| Utanuzi wa Mtandao wa Maji hadi Nyashimba, Nyigogo, Ilula, Mwabasabina Magu Mjini | 149.33 | | | 30 Juni 2020 |
| Utanuzi wa mtandao wa maji hadi Lumeji na Bundilya | | | 159.03 | 30 Juni 2022 |
| Utanuzi wa mtandao wa maji hadi Buhumbi na Mwalina | | 94.86 | | 30 Juni 2021 |
| Utanuzi wa mtandao wa maji hadi Shinembo na Misungwi | | 183.70 | 102.30 | 30 Juni 2022 |
| Utanuzi wa mtandao wa maji hadi Kahangala | 42.28 | | 133.92 | 30 Juni 2022 |
| Kununua Pikipiki 2 | | 2.00 | 2.00 | 30 Juni 2022 |
| Kununua pikipiki ya miguu mitatu (Bajaj) | | 5.00 | | 30 Juni 2021 |

| Kazi Zitakazofanywa | Shilingi Milioni | | | Mwisho wa Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | |
| Kununua kompyuta 7 | 1.50 | 3.00 | 3.00 | 30 Juni 2022 |
| Kununua printa moja | 0.90 | 1.50 | 2.00 | 30 Juni 2022 |
| Kununua dira 70 za malipo ya kabla | | 9.00 | 22.50 | 30 Juni 2022 |
| Kuunganisha wateja wapya 1000 | 21.62 | 34.80 | 139.20 | 30 Juni 2022 |
| Kununua viungio kwa ajili ya ukarabati n amatengenezo | 13.08 | | | 30 Juni 2020 |
| Kununua *Potable Butt Fussion Machine* moja | 3.50 | | | 30 Juni 2020 |
| Kununua majenereta 4 na vifaa vyake kwa *ajili Potable ButtFussion Machine* | 2.70 | 2.20 | 5.91 | 30 Juni 2022 |
| Jumla (UwekezajiMpya) | 234.92 | 507.49 | 903.73 | |
| JUMLA KUU | 250.00 | 530.00 | 930.00 | |

JEDWALI LA TATU

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(c))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

| Maelezo | Kipimo | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Idadi ya wateja wapya wa majisafi | Na | 210 | 157 | 248 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 35 | 30 | 28 |
| Wateja wenye dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 90 | 95 |

JEDWALI LA NNE

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya ..........)*

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (Milioni TZS)

| GHARAMA | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| | Zilizoidhinishwa | Zilizoidhinishwa | Zilizoidhinishwawa |
| Uzalishajiwa Maji | 418.56 | 424.52 | 453.30 |
| Usambazajiwa Maji | 18.00 | 18.74 | 19.51 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Matengenezo | 174.00 | 264.45 | 264.45 |
| Watumishi | 301.82 | 358.42 | 392.84 |
| Utawala | 50.82 | 71.87 | 83.92 |
| Matangazo | 5.00 | 5.21 | 5.42 |
| Matukio | 6.75 | 7.85 | 8.95 |
| Gharama za Benki | 0.90 | 0.94 | 0.98 |
| Jumla (Uendeshaji na Matengenezo) | 975.85 | 1151.99 | 1229.36 |
| Uchakavu | 273.50 | 550.00 | 938.00 |
| Jumla ya Gharama Zote | 1,249.35 | 1,701.99 | 2,167.36 |
| Toa: Mapatomengineyo | 13.10 | 11.36 | 15.66 |
| Mapato yatokanayo na mauzo ya maji | 1,236.25 | 1,690.63 | 2,151.70 |

Dodoma NZINYANGWA E. MCHANY

............................. 2019 *Mkurugenzi Mkuu*